# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

**04 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**KIKAO CHA THELATHINI NA TISA - TAREHE 04 JUNI, 2025**

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**498 MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itazipatia fedha za ukarabati Shule kongwe za Msingi Makanya na Kwai katika Jimbo la Lushoto.

**499 MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA MULAMULA (KUTEULIWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuanza ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya kimkakati ya Kyazi Kayanga - Misenyi.

**500 MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini sababu ya Wilaya ya Nkasi kukosa miradi ya kimkakati.

**501 MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa majengo mapya ya Kituo cha Afya cha Kamsamba – Momba.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**502 MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwa nini Serikali isiagize CAG akague URA SACCOS ya Jeshi la Polisi.

**503 MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Polisi na Gari la Zimamoto katika Wilaya ya Kyerwa inayopakana na nchi mbili ili kukabiliana na majanga ya moto.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**504 MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, jitihada gani zimefanyika kurahisisha upatikanaji wa *VISA* kwa Watalii wenye uraia tofauti wanaokuja nchini kwa mwitikio wa *Royal Tour*.

## WIZARA YA KILIMO:

**505 MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, jitihada zipi zinafanywa na Serikali kuhakikisha Wilaya ya Ludewa inajengewa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

## WIZARA YA MAJI:

**506 MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unapunguza changamoto ya maji.

**507 MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini maji kutoka Ziwa Victoria yatafika katika Vijiji vya Sirari, Nyamwaga na Nyamongo vilivyopo Tarime Vijijini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**508 MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami Km 42 barabara inayoelekea Makao Makuu ya Wilaya Mkalama.

**509 MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu na kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Nyoni – Maguu.

**510 MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya kutoka Kilindoni - RAS Mkumbi - Mafia yenye Km 52.16 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**511 MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ipo katika hatua gani ya ujenzi wa kipande cha Barabara kutoka Katoro hadi Daraja la Nyikonga kwenye Barabara ya Katoro – Ushirombo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**04 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**

BUNGE LA TANZANIA
PARLIAMENT OF TANZANIA